07

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## JULAI, 2026

**19 AGOSTI, 2026**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA JULAI, 2026

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hapa Zanzibar. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA YALIYORIPOTIWA POLISI JULAI 2026


Jumla ya matukio 138 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Julai, 2026 ambapo waathirika walikuwa 138. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 118 sawa na asilimia 85.5), wakifuatiwa na wanawake 19 (asilimia 13.8) na mwanaume alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.7. Miongoni mwa waathirika watoto 118, wasichana walikuwa 95 (asilimia 80.5) na wavulana walikuwa 23 sawa na asilimia 19.5 ya waathirika watoto wote.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia, Julai 2026**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 62, ambapo waathirika 58 walikuwa wasichana na wanne (4) wanawake. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa 18 ambapo waathirika wote walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 11 ambapo waathirika 10 walikuwa wasichana na mmoja (1) alikuwa mwanamke. Matukio ya kutorosha yalikuwa 17 ambapo waathirika 16 walikuwa wasichana na mwathirika mmoja (1) alikuwa mwanamke. Matukio ya lugha ya matusi yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika watatu (3) walikuwa wanawake, waathrika wawili (2) walikuwa wasichana na waathirika wanne (4) walikuwa wavulana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 17 ambapo waathirika nane (8) walikuwa wanawake, waathirika nane (8) walikuwa wasichana na mwathirika mmoja (1) alikuwa mvulana. Tukio la kutupa watoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika ni msichana. Tukio la mauaji lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamme, na matukio ya kumpa na kupokea ujauzito yalikuwa mawili (2) ambapo waathirika wote walikuwa wanawake.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Julai, 2026**



Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na matukio mengi (matukio 32) zikifuatia Wilaya ya Mjini na Magharibi ‘B’ ambapo kumeripotiwa matukio 24 kwa kila wilaya. Wilaya ya Kusini na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio(matukio 4 kwa kila wilaya).

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Julai, 2026**



Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 3.5 kufikia matukio 138 kwa mwezi Julai, 2026 ikilinganishwa na matukio 143 yaliyoripotiwa mwezi wa Juni, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Julai, 2026 yalikuwa kutupa watoto, kulawiti/kunajisi, kutorosha, na shambulio la aibu/kukashifu. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa(matukio 32) ya matukio kwa mwezi wa Julai, 2026 na Wilaya ya Magharibi 'B' ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Juni, 2026 (matukio 26).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2026 na Julai, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu kubaka | | Kutupa watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 |
| Kaskazini 'A' | 13 | 5 | 9 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 18 | 10 | 10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini | 3 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 23 | 24 | 12 | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 3 | 2 | 0 |
| Magharibi 'A' | 24 | 32 | 9 | 17 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 5 | 3 | 2 | 3 | 3 |
| Magharibi 'B' | 26 | 24 | 13 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 6 | 6 | 0 | 1 |
| Wete | 8 | 18 | 5 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 6 |
| Micheweni | 4 | 7 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Chake Chake | 12 | 5 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 4 |
| Mkoani | 8 | 4 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **143** | **138** | **78** | **62** | **0** | **0** | **0** | **1** | **13** | **18** | **13** | **11** | **9** | **17** |

**Inaendelea....Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Juni 2026 na Julai, 2026**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya Matusi | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Watoto | | Mauaji | | Kuingilia Maharimu | | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Shambulio la Mtoto | |
| | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 | Juni 2026 | Julai 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 3 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **9** | **9** | **15** | **17** | **1** | **0** | **2** | **1** | **1** | **0** | **2** | **2** | **0** | **0** |

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 29.0 na kufikia matukio 138 kwa mwezi Julai, 2026 kutoka matukio 107 yaliyoripotiwa mwezi wa Julai, 2025. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Julai, 2026 isipokuwa matukio ya wizi wa watoto. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Julai, 2026 (matukio 32) na mwezi wa Julai, 2025 (matukio 26).

**Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Julai 2025 na Julai 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kutupa Watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 |
| Kaskazini 'A' | 6 | 5 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 5 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kati | 16 | 10 | 12 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini | 3 | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 12 | 24 | 8 | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 26 | 32 | 9 | 17 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 5 | 3 | 2 | 4 | 3 |
| Magharibi 'B' | 14 | 24 | 7 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 1 | 6 | 2 | 1 |
| Wete | 11 | 18 | 6 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| Micheweni | 2 | 7 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Chake Chake | 9 | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 4 |
| Mkoani | 1 | 4 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **138** | **57** | **62** | **0** | **0** | **0** | **1** | **11** | **18** | **6** | **11** | **12** | **17** |

Inaendelea....Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Julai 2025 na Julai 2026

| Wilaya | Aina ya Matukio ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Wizi wa watoto | | Mauaji | | Kuingilia maharimu | | Kumpa na kupokea ujauzito | | Uzinifu | | Usumbufu wa kingono | |
| | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 |
| Kaskazini 'A' | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **17** | **17** | **1** | **0** | **0** | **1** | **0** | **0** | **0** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Miongoni mwa waathirika watoto 118 waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 58, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana 18, kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 10, kutorosha walikuwa wasichana 16, shambulio la aibu/kukashifu wasichana walikuwa nane (8) na mvulana mmoja (1), lugha ya matusi wasichana wawili (2) na wavulana wanne (4) na kutupa watoto alikuwa msichana mmoja (1).

Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Julai, 2026

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutupa Mtoto | | Kutelekeza Watoto | | Shambulio la mtoto | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 21 | 12 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 29 | 17 | 5 | 1 | 3 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 22 | 8 | 2 | 6 | 1 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 16 | 9 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 5 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **118** | **58** | **18** | **10** | **16** | **0** | **2** | **4** | **8** | **1** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 19 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa wanne (4), Kuingilia kinyume na maumbile, alikuwa mmoja (1), kutorosha alikuwa mmoja(1), Lugha ya matusi watatu (3), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa nane (8) na Kumpa na kupokea ujauzito walikuwa wawili (2).

**Jadweli 1.5: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Julai, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Lugha ya Matusi | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Uzinifu |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **19** | **4** | **1** | **1** | **3** | **8** | **2** | **0** |

Kwa mwezi wa Julai 2026, idadi ya muaathirika alikuwa mmoja(1), ambae mwanamme kwa tukio la mauaji.

Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Julai, 2026

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Lugha ya Matusi | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Mauaji | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Wizi wa Watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1** | **0** | **0** | **0** | **1** | **0** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 56) sawa na asilimia 47.5 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 36) sawa na asilimia 30.5. Matukio 18 sawa na asilimia 15.3 yaliripotiwa kwa umri wa miaka 6-10 na umri wa miaka 0-5, yaliripotiwa matukio nane (8) sawa na asilimia 6.8. Aidha idadi kubwa ya matukio ya kubaka yameripotiwa umri wa miaka 15-17 (matukio 36) sawa na asilimia 62.1 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.7: Aina ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Julai, 2026**

| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 2 | | 5 | | 15 | | 36 | | 58 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 3 | | 8 | | 5 | | 2 | | 18 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 5 | | 3 | | 2 | | 10 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 11 | 0 | 16 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 3 | 2 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 1 | 2 | 0 | 8 | 1 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **5** | **3** | **10** | **8** | **29** | **7** | **51** | **5** | **95** | **23** |

Idadi ya matukio ya watoto waliopitia udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 3.3 kufikia matukio 118 kwa mwezi wa Julai 2026 ikilinganishwa na matukio 122 yaliyoripotiwa mwezi wa Juni 2026. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Julai 2026 ni matukio ya kutupa watoto,kulawiti/kunajisi na kutorosha.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Juni, 2026 na Julai, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kutupa Watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Lugha ya Matusi | | Kutelekeza Watoto | | Shambulio la Mtoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 | Juni - 26 | Julai - 26 |
| 0-5 | 1 | 2 | 0 | 1 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 8 | 8 |
| 6-10 | 1 | 5 | 0 | 0 | 1 | 8 | 2 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 18 |
| 11-14 | 15 | 15 | 0 | 0 | 6 | 5 | 2 | 3 | 4 | 4 | 4 | 6 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 | 36 |
| 15-17 | 54 | 36 | 0 | 0 | 2 | 2 | 7 | 2 | 5 | 11 | 5 | 2 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 78 | 56 |
| **Jumla** | **71** | **58** | **0** | **1** | **11** | **18** | **13** | **10** | **9** | **16** | **11** | **9** | **6** | **6** | **1** | **0** | **0** | **0** | **122** | **118** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 24.2 na kufikia matukio 118 kwa mwezi wa Julai 2026 ikilinganishwa na matukio 95 yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Julai 2025. Matukio yaliyoripotiwa kupungua kwa mwezi Julai 2026 ikilinganishwa na Julai 2025 ni matukio ya shambulio la aibu/kukashifu na usumbufu wa kingono.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Julai, 2025 na Julai, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Lugha ya Matusi | | Kutupa Watoto Watoto | | Usumbufu wa Kingono | | Kutelekeza Watoto | | Shambulio la Mtoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 | Julai - 25 | Julai - 26 |
| 0-5 | 0 | 2 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 8 |
| 6-10 | 5 | 5 | 6 | 8 | 2 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 18 |
| 11-14 | 11 | 15 | 3 | 5 | 4 | 3 | 4 | 4 | 7 | 6 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 29 | 36 |
| 15-17 | 38 | 36 | 0 | 2 | 0 | 2 | 8 | 11 | 2 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 48 | 56 |
| **Jumla** | **54** | **58** | **11** | **18** | **6** | **10** | **12** | **16** | **11** | **9** | **0** | **6** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **95** | **118** |

Matukio mengi (matukio 67) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 48.6 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 26) sawa na asilimia 18.8 na vichakani (matukio 18) sawa na asilimia 13.0 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Julai 2026.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Julai, 2026**





Matukio 117 kati ya matukio 138 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 84.8 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 17 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 12.3) na matukio manne (4) yamefungwa na polisi (asilimia 2.9).

**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Julai, 2026**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | Waathirika | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto | | Watu Wazima | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | | | | | | | |
| Kubaka | 62 | 58 | | 4 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 51 | 0 |
| Kulawiti/Kunajisi | 18 | | 18 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 14 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 11 | 10 | | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 7 | 0 |
| Kutorosha | 17 | 16 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 15 | 0 |
| Lugha ya matusi | 9 | 2 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 17 | 8 | 1 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 |
| Mauaji | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **138** | **95** | **23** | **19** | **1** | **0** | **0** | **0** | **4** | **17** | **117** | **0** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Julai 2026 walikuwa 138 kati yao 55 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 39.9, watu wasiojulikana walikuwa 44 sawa na asilimia 31.9, Jirani walikuwa 30 sawa na asilimia 21.7 na watu wengine walikuwa tisa (9) sawa na asilimia 6.5.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Julai, 2026**



## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI KWA WATU WENYE ULEMAVU, JULAI 2026

Jumla ya watu watatu(3) wenye ulemavu wamefanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Julai 2026. Ambapo mwanamke alikuwa mmoja(1) na mvulana mmoja (1) ambao wote ni walemavu wa akili.

**Jadweli 1.11: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu kwa Wilaya na Jinsi, Julai 2026**

| Wilaya | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **0** | **1** | **3** |

Muathirika wa wa ubakaji alikuwa mmoja (1) , kulawiti alikuwa mmoja(1) na  shambuluo la aibu/kukashifu mmoja(1).

**Jadweli 1.12: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu kwa Jinsi, Julai 2026**

| Jinsi | Kubaka | Kulawiti | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 1 | [redacted] | 1 | 2 |
| Mvulana | [redacted] | 1 | [redacted] | 1 |
| **Jumla** | **1** | **1** | **1** | **3** |

## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR JULAI, 2026

Jumla ya Majalada 67 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Julai, 2026 ambayo yalihusisha makosa 70. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 51) sawa na asilimia 72.9 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Julai, 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 2 | 2 |
| Kusini Unguja | 8 | 8 |
| Mjini Magharibi | 48 | 51 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 3 |
| Kusini Pemba | 6 | 6 |
| Makao Makuu | 0 | 0 |
| **Jumla** | **67** | **70** |

Kati ya Majalada 67 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Julai, 2026, majalada 16 hayajatolea uamuzi, majalada 26 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada 23 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada mawili (2) yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Julai 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini Unguja | 8 | 3 | 0 | 0 | 5 |
| Mjini Magharibi | 48 | 14 | 1 | 23 | 10 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 6 | 5 | 1 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **67** | **26** | **2** | **23** | **16** |

Miongoni mwa makosa 67 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi Julai 2026, makosa mengi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 41) sawa na asilimia 58.6 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Julai 2026**

| Mkoa | Jumla ya makosa kwenye majalada yaliopokelewa | Kutorosha | Udhalilishaji Mkubwa wa Kingono | Kubaka | Kumuingilia Maharimu | Kulawiti | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kukashifu kwa njia ya Mtandao |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 8 | 0 | 0 | 6 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini Magharibi | 51 | 2 | 0 | 29 | 0 | 6 | 6 | 7 | 1 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 6 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Makao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **70** | **3** | **1** | **41** | **1** | **7** | **8** | **8** | **1** |

## MASHAURI NA MAKOSA YA  UDHALILISHAJI YALIYOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA JULAI 2026

Jumla ya mashauri 40 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Julai, 2026, ambapo yamehusisha makosa 50. Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri 28 yaliyohusisha makosa 37 ya udhalilishaji wa kijinsia sawa na asilimia  79.0 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Julai, 2026**




Kati ya mashauri 40 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar,  mashauri 38 bado yanaendelea sawa na asilimia 95.0 na mashauri mawili(2)  yametiwa hatiani sawa na asilimia 5.0.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Mashauri ya Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Julai 2026**

| Aina ya Makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa hatiani | | | | | Zisizo na hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachi wa huru | Zilizoondoshwa/ Zilozofutwa |
| Kubaka | 18 | 17 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka na kutorosha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Udhalilishaji mkubwa wa kingono | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **40** | **38** | **0** | **2** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

Jumla ya makosa 50 yaliyopokelewa katika Mahakama za udhalilishaji wa kijinsia, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 26) sawa na asilimia 52.0 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa Julai, 2026**

| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 2 | 4 | 18 | 0 | 2 | 26 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 13 | 0 | 0 | 13 |
| Kulawiti | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 4 |
| kutorosha | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 4 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Udhalilishaji Mkubwa wa kingono | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **3** | **6** | **37** | **1** | **3** | **50** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 138 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Julai, 2026 ambapo waathirika walikuwa 138. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 118 sawa na asilimia 85.5), wakifuatiwa na wanawake 19 (asilimia 13.8) na mwanaume alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.7.

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 3.5 kufikia matukio 138 kwa mwezi Julai, 2026 ikilinganishwa na matukio 143 yaliyoripotiwa mwezi wa Juni, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Julai, 2026 yalikuwa kutupa watoto, kulawiti/kunajisi, kutorosha, na shambulio la aibu/kukashifu. Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na idadi kubwa(matukio 32) ya matukio kwa mwezi wa Julai, 2026 na Wilaya ya Magharibi ‘B’ ilikuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Juni, 2026 (matukio 26).

Matukio 117 kati ya matukio 138 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 84.8 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 17 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 12.3) na matukio manne (4) yamefungwa na polisi (asilimia 2.9).

Jumla ya Majalada 67 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Julai, 2026 ambayo yalihusisha makosa 70. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 51) sawa na asilimia 72.9 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine. Kati ya Majalada 67 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Julai, 2026, majalada 16 hayajatolea uamuzi, majalada 26 yameruhusiwa kwenda mahakamani, majalada 23 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada mawili (2) yamependekezwa kufungwa.

Jumla ya mashauri 40 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Julai, 2026, ambapo yamehusisha makosa 50 . Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri 28 yaliyohusisha makosa 37 ya udhalilishaji wa kijinsia sawa na asilimia 79.0 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine. Kati ya mashauri 40 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri 38 bado yanaendelea sawa na asilimia 95.0 na mashauri mawili (2) yametiwa hatiani sawa na asilimia 5.0.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Julai, 2026**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Majumba mabovu | | Vichakani | | Sehemu nyengine | | Sehemu za kazi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 0 | | 38 | | 5 | | 11 | | 7 | | 1 | | 0 | | 62 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 1 | | 5 | | 0 | | 8 | | 3 | | 1 | | 0 | | 18 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 6 | | 0 | | 3 | | 2 | | 0 | | 0 | | 11 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 9 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 |
| Lugha ya matusi | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 3 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 16 | 1 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Ukatili wa mtoto/Mtu wenye ulemavu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **6** | **4** | **61** | **6** | **11** | **0** | **17** | **9** | **15** | **3** | **4** | **2** | **0** | **0** | **114** | **24** |

**Jadweli 2.0: Idadi ya Waaathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya kwa Aina ya Matukio na Wilaya Julai, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kujaribu Kubaka | Kutorosha | | Lugha ya Matusi | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Uzinifu | |
| | | W'ke | W'me | W'me | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me |
| Kaskazini 'A' | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 10 | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 24 | 12 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 32 | 17 | 5 | 2 | 0 | 3 | 0 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 24 | 8 | 2 | 6 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 18 | 10 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 7 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **138** | **62** | **18** | **11** | **0** | **17** | **0** | **5** | **4** | **16** | **1** | **0** | **1** | **1** | **0** | **2** | **0** | **0** | **0** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Juni, 2026 na Julai, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Juni-2026 | Julai-2026 | Juni-2026 | Julai-2026 | Juni-2026 | Julai-2026 | Juni-2026 | Julai-2026 | Juni-2026 | Julai-2026 |
| Kubaka | 78 | 62 | 7 | 4 | 71 | 58 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 13 | 18 | | | | | 11 | 18 | 2 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 13 | 11 | 0 | 1 | 13 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 9 | 17 | 0 | 1 | 9 | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 9 | 9 | 3 | 3 | 2 | 2 | 4 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 17 | 4 | 8 | 9 | 8 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Kutupa watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **143** | **138** | **17** | **19** | **105** | **95** | **17** | **23** | **4** | **1** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Julai, 2025 na Julai, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 | Julai-2025 | Julai-2026 |
| Kubaka | 57 | 62 | 3 | 4 | 54 | 58 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 11 | 18 | | | | | 11 | 18 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 6 | 11 | 0 | 1 | 6 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 12 | 17 | 0 | 1 | 12 | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 3 | 9 | 3 | 3 | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 17 | 17 | 5 | 8 | 10 | 8 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Kutupa watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wizi wa watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **138** | **11** | **19** | **83** | **95** | **12** | **23** | **1** | **1** |

**Jadweli 5.0 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Julai 2026**

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 3 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 4 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Lugha ya matusi | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 5 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Jumla | **14** | **0** | **4** | **0** | **0** | **0** | **1** | **1** | **1** | **0** | **19** | **1** |

**Jadweli 6.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea kwa Jinsi; Julai, 2026**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** |
| Kubaka | 2 | | 4 | | 9 | | 14 | | 25 | | 7 | | 1 | | 0 | | 62 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 1 | | 3 | | 5 | | 6 | | 1 | | 0 | | 0 | | 18 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 1 | | 3 | | 5 | | 2 | | 0 | | 0 | | 11 | |
| Kutorosha | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 2 | 0 | 5 | 0 | 4 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 16 | 1 |
| Mauaji | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **7** | **3** | **8** | **1** | **16** | **4** | **27** | **8** | **45** | **7** | **9** | **1** | **2** | **0** | **0** | **0** | **114** | **24** |

**Jadweli 7: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Miezi , 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 116 | 122 | 65 | 173 | 171 | 103 | 113 |
| Februari | 155 | 100 | 100 | 164 | 175 | 107 | 98 |
| Machi | 136 | 141 | 82 | 155 | 125 | 78 | 103 |
| Aprili | 95 | 108 | 68 | 148 | 148 | 102 | 129 |
| Mei | 118 | 66 | 74 | 154 | 172 | 107 | 128 |
| Juni | 102 | 97 | 97 | 127 | 174 | 97 | 143 |
| Julai | 114 | 108 | 78 | 168 | 165 | 107 | 138 |
| Agosti | 116 | 96 | 131 | 175 | 157 | 116 | |
| Septemba | 115 | 90 | 170 | 157 | 148 | 106 | |
| Oktoba | 103 | 107 | 164 | 199 | 147 | 99 | |
| Novemba | 92 | 90 | 177 | 172 | 136 | 107 | |
| Disemba | 101 | 97 | 154 | 162 | 91 | 99 | |
| **Jumla** | **1,363** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** | **1,228** | **852** |

**Jadweli 8: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Miezi na Wilaya, 2026**

| Miezi | Kaskazini 'A' | Kaskazini 'B' | Kati | Kusini | Mjini | Magharibi 'A' | Magharibi 'B' | Wete | Micheweni | Chake Chake | Mkoani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 5 | 7 | 9 | 2 | 18 | 23 | 18 | 11 | 9 | 6 | 5 | 113 |
| Februari | 3 | 5 | 10 | 2 | 18 | 21 | 17 | 7 | 6 | 7 | 2 | 98 |
| Machi | 8 | 9 | 10 | 1 | 17 | 19 | 18 | 11 | 2 | 6 | 2 | 103 |
| Aprili | 8 | 7 | 10 | 3 | 25 | 23 | 21 | 9 | 3 | 10 | 10 | 129 |
| Mei | 6 | 8 | 13 | 2 | 20 | 25 | 24 | 12 | 4 | 6 | 8 | 128 |
| Juni | 13 | 4 | 18 | 3 | 23 | 24 | 26 | 8 | 4 | 12 | 8 | 143 |
| Julai | 5 | 5 | 10 | 4 | 24 | 32 | 24 | 18 | 7 | 5 | 4 | 138 |
| Agosti | | | | | | | | | | | | |
| Septemba | | | | | | | | | | | | |
| Oktoba | | | | | | | | | | | | |
| Novemba | | | | | | | | | | | | |
| Disemba | | | | | | | | | | | | |
| **Jumla** | **48** | **45** | **80** | **17** | **145** | **167** | **148** | **76** | **35** | **52** | **39** | **852** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia ni Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu,kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mtu, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake, wanaume na watoto na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Sheria ya mwenendo wa makosa ya Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesizinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi zaidi Tafadhali Wasiliana na:-**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**